# MFAHAMU

# YESU

# ALIVYO

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha  MFAHAMU YESU ALIVYO. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

MFAHAMU YESU ALIVYO.

1.Masihi (kristo)…………………………………………………..1

2. Mwana wa Mungu…………………………………………..2

3. Mtenda Miujiza ………………………………………3-6

4. Mponyaji………………………………………………………….7

5. Mwalimu (Rabi)…………………………………………………..8

6. Nabii (Mwonaji)……………………………………………………9

7. Mwenye amri ya kutoa pepo na nguvu zingine za giza…………………………………………………………… 10

8.Hana dhambi……………………………………………………..11

9.Anasema ……………………………………………………………12

10.Amejaa Amani,Furaha,Upendo,Haki………………13

13.Amejaa Uzima tele……………………………………..14

14.Mfalme…………………………………………………………15-16

15.Kuokoka…………………………………………………………..17

16. Mwisho……………………………………………………………18

## 1. MASIHI (kristo)

Yesu ni masihi yaani kristo. Ni mpakwa mafuta wa mungu aliyetabiriwa na manabii na kushuhudiwa na malaika kuwa ndiye atakayewaokoa  watu na dhambi zao .

**Math 1:41 "Huyo akamwona kwanza Simoni, ndugu yake mwenyewe, akamwambia, Tumemwona Masihi (maana yake, Kristo)."** Ktk maandiko hayo hapo juu waisraeli walikuwa wakimsubiri masihi waliyeahidiwa na mungu kuwa ndiye mfalme.Simon ni miongoni mwa misraeli aliyeamini kuwa Yesu ni masihi. Wewe je waamini? **Math 4:25 - 26   "Yule mwanamke akamwambia, Najua ya kuwa yuaja Masihi, (aitwaye Kristo); naye atakapokuja, yeye atatufunulia mambo yote. Yesu akamwambia, Mimi ninayesema nawe, ndiye."** Mwanamke msamaria ijapokuwa alikuwa mwenye dhambi habari za ujio wa masihi alikuwa nazo aliamini ndiye angeliwafunulia mambo yote ya mungu yaliyofichika wasiyoyajua. Na Yesu anakiri wazi kuwa yeye ndiye huyo masihi wanayemsubiria kwa wokovu wao. Yesu ni masihi kwa neno la kinywa chake.  **Math 10.24 — 25 "Basi Wayahudi walimzunguka, wakamwambia, Hata lini utatuhangaisha nafsi zetu? Kama wewe ndiwe Kristo, utuambie waziwazi.Yesu akawajibu, Naliwaambia, lakini ninyi hamsadiki. Kazi hizi ninazozifanya kwa jina la Baba yangu ndizo zinazonishuhudia."** Ktk maandiko haya wayahudi walihangaika nafsini mwao wakijiuliza kuwa huyu ni kristo kwa sababu hawakumwamini alipowaambia. Ndipo akawasaidia kutokuamini kwao kwa kuwataka watazame na kuzitafakari kazi anazozifanya kwa jina la Baba ya kuwa ni za mungu zinamfunua Yesu ndiye Kristo. **Mahali Yesu alipo** kazi za mungu alizozitenda zi Dhahiri hata leo Mf:miuzija,ponyaji ,mafundisho,nabii pamoja kutolewa kwa pepo na nguvu za giza.Hayo huyatenda kwa kutumia watumishi wake aliowatuma au aliowapeleka. Hao ni Mitume,manabii,waandishi,Wachungaji,Wainjilisti,Walimu,Waponyaji, WatendaMiujiza,Wahubiri wa Injili. n.k

## 2.MWANA WA MUNGU

Yesu ni mwana wa Mungu yaani ni mtoto wa kiume wa Mungu ; Mungu ni babaye alikuwako mbinguni kabla ya kuja duniani kwa kuzaliwa na bikira mariamu kiumiujzwa kuja kuwaokoa wanadamu na dhambi zao.

**Math 16.16 "Simoni Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."**

Ktk maandiko haya Petro akiri kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu. Yesu alimwambia umefunuliwa na Baba yangu (Mungu) kuwa mimi ni mwanaye tena kristo wa kweli aliyenituma kuja ulimwenguni kuyatimiliza yaliyonenwa na manabii juu ya kristo na kutenda mapenzi ya mungu. Mungu amfunua Yesu ni mwanaye wa kiume mbele za mitume kwa kumtumia Petro.

**Math 17.5 "Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye."**

Ktk maandiko haya mungu anafunua Yesu ni mwanaye wa kiume mbele za mitume kwa sauti yake iliyodhahiri aliyosema ikasikiwa na mitume waliokuwa karibu na Yesu.

**Luk 1:30—35 "... Litakuwaje neno hili, maana sijui mume?Malaika akajibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu." .**

Ktk maandiko hayo hapo malaika anashuhudia Yesu ni mwana wa mungu kabla hajazaliwa.Fahamu neno hili mwana wa mwanadamu ni mwanadamu,mwana wa kondoo ni kondoo halikadharika mwana wa mungu ni mungu. Yesu ni Mungu kwa kuwa ni mwana wa Mungu.Mwadamu hazai kondoo na kondoo hazai mbuzi kama una masikio ya kusikia na usikie. Yesu ni mungu je waamini?

## 3. MTENDA MIUJIZA

Miujiza ni nini? Miujiza ni matendo makuu ya Mungu atendayo ktk mwili wa mtu au vitu viliumbwa naye au kutengenezwa na mtu.

Mfano wa miujiza ktk mwili wa mtu ile ya ufufuo (kufufuliwa mtu aliyekufa mwenye siku zisizozidi nne au seli za kilema au kiwete ),kurejeshewa kiungo kilichopotea au kukatwa(muujiza wa kurejeshewa pina mpya,mguu,vidole,titi lililokatwa kwa sababu ya kansa au figo). Yesu ni mtenda hiyo miujiza na Baba yake.

**Yohana 2.3 — 10**

**"Hata divai ilipowatindikia, mamaye Yesu akamwambia, Hawana divai.Yesu akamwambia, Mama, tuna nini mimi nawe? ...Yesu akawaambia, Jalizeni mabalasi maji. Nao wakayajaliza hata juu. Akawaambia, Sasa tekeni, mkampelekee mkuu wa meza. Wakapeleka.**

**Naye mkuu wa meza alipoyaonja yale maji yaliyopata kuwa divai, (wala asijue ilikotoka, lakini watumishi walijua, wale walioyateka yale maji), yule mkuu wa meza alimwita bwana arusi,akamwambia, Kila mtu kwanza huandaa divai iliyo njema; hata watu wakiisha kunywa sana ndipo huleta iliyo dhaifu; wewe umeiweka divai iliyo njema hata sasa."**

Ktk maandiko hapo juu , Yesu alibadili maji kuwa divai huu ni mfano wa muujiza wa ktk vitu (maji&divai) vilivyoumbwa na mungu . Yesu ni mtenda miujiza anaweza kubadili kitu kutoka ktk umbo moja kwenda jingine mfano maji kuwa divai,maziwa au damu, jiwe kuwa mkate,Yesu hafanya miujiza kwa kuwafanya wale wasioamini mungu wapate kumwamini nakuziona nguvu zake kupitia hiyo miujiza hivyo kudumu ktk kushika mafundisho,amri na maagizo yake.

# 4. MTENDA MIUJIZA

**Yoh 6:5—9**

**“Basi Yesu alipoinua macho yake akaona mkutano mkuu wanakuja kwake, alimwambia Filipo, Tununue wapi mikate, ili hawa wapate kula? Na hilo alilinena ili kumjaribu; kwa maana alijua mwenyewe atakalotenda. Filipo akamjibu, Mikate ya dinari mia mbili haiwatoshi, kila mmoja apate kidogo tu.Wanafunzi wake mmojawapo, Andrea, nduguye Simoni Petro, akamwambia, Yupo hapa mtoto, yuna mikate mitano ya shayiri na samaki wawili, lakini hivi ni nini kwa watu wengi kama hawa? Yesu akasema, Waketisheni watu. Na mahali pale palikuwa na majani tele. Basi watu waume wakaketi, wapata elfu tano jumla yao. Basi Yesu akaitwaa ile mikate, akashukuru, akawagawia walioketi; na kadhalika katika wale samaki kwa kadiri walivyotaka.Nao waliposhiba, aliwaambia wanafunzi wake, Kusanyeni vipande vilivyobaki, kisipotee cho chote.Basi wakavikusanya, wakajaza vikapu kumi na viwili, vipande vya mikate mitano ya shayiri vilivyowabakia wale waliokula”**

Yesu alitenda muujiza wa kuongeza samaki na mikate michache na kulisha wanaume wapatao elfu tano huu ni mfano wa muujiza ktk vitu vilivyombwa naye.Yesu anaweza kuongeza vitu vikaongezeka kukidhi uhitaji mfano chakula, pesa,nguo n.k  Yesu hutenda miujiza ili kuwa fanya wasioamini wapate kumwamini wale wamfuatao na kulitukuza jina la Baba yake.

Mahali popote ilipo miujiza Yesu yupo hapo na mungu yupo hapo. Huduma au kanisa la waliokoka ambao watumishi wake hutumiwa na Mungu na Yesu kutenda miujiza ufahamu Yesu yupo hapo na mungu pia .Uogope kutenda dhambi usiwe mwenye mashaka  Uwe mwenye kutafakari na kukumbuka miujiza ya Yesu ukapate hekima na  kushukuru ukaibebe ndani ya moyo wako itakusaidia siku ya uhitaji wako.

## 5. MTENDA MIUJIZA

Yoh 6.17 - 21

**" Wakapanda chomboni, wakaanza kuivuka bahari kwenda Kapernaumu. Nako kumekwisha kuwa giza, wala Yesu hajawafikia.Na bahari ikaanza kuchafuka kwa kuvuma upepo mkuu.Basi wakavuta makasia kadiri ya maili tatu nne, wakamwona Yesu anakwenda juu ya bahari na kukikaribia chombo; wakaogopa.Naye akawaambia, Ni mimi, msiogope.Basi wakataka kumpokea chomboni; na mara hiyo chombo kikaifikilia nchi waliyokuwa wakiiendea."**

Yesu alitenda muujiza wa kutembea juu ya bahari yaani maji. Mfano pia wa muujiza wa ktk vitu alivyoviumba mungu. Alifanya hayo mbele za mitume kumi na mbili ili aimarishe Imani yao kwake ili wadumu kumfuata na kumwamini ya kuwa ndiye kristo mbele ya safari yapo mambo mazuri aliyowaandalia.

**Luk 8: 22 — 25 Wakamwendea, wakamwamsha, wakisema, Bwana mkubwa, Bwana mkubwa, tunaangamia. Akaamka, akaukemea upepo na msukosuko wa maji, vikakoma; kukawa shwari.Akawaambia, Imani yenu iko wapi? Wakaogopa, wakamaka, wakisema wao kwa wao, Ni nani huyu basi hata anaamuru upepo na maji, navyo vyamtii?**

Yesu alitenda muujiza wa kutiisha upepo na maji. Na huu ni mfano wa muujiza wa ktk vitu alivyoumba Mungu. Miujiza asili yake ni mbinguni na kwa Baba yake Yesu yaani Mungu aliyeandikwa ktk kitabu cha Mwanzo ktk biblia kinachozungumzia uumbaji wa Adamu.

Yesu sikuzote hupenda kuona wale wamwaminio na kumfuata Imani yao wanaiweka kwake.Miujiza ya Mungu inawezekana kwake yeye aaminiye. Miujiza ni sehemu ya maisha ya Yesu alipoishi ktk dunia hii,

## 6. MTENDA MIUJIZA

Yoh 11

**“... Naye akiisha kusema hayo, akalia kwa sauti kuu, Lazaro, njoo huku nje. Akatoka nje yule aliyekufa, amefungwa sanda miguuni na mikononi, na uso wake amefungwa leso. Naye Yesu akawaambia, Mfungueni, mkamwache aende zake. Basi wengi katika Wayahudi waliokuja kwa Mariamu, na kuyaona yale aliyoyafanya, wakamwamini.”**

Yesu alitenda Muujiza wa kumfufua lazaro aliyekaa kaburi siku nne. Huu ni mfano wa muujiza ktk mwili aliouumba Mungu mwili wa lazaro. Yesu ana nguvu ya kufufua vilivyokufa hata seli za miguu ya kiwete au mlemavu zilizokufa akazipa uhai mpya. Lakini pia Yesu anaweza kufufua na roho pia kama sivyo kuokoka kusingewezekana maana ni muujiza tupu.

**Math 17.27 “Lakini tusije tukawakwaza, enenda baharini ukatupe ndoana, ukatwae samaki yule azukaye kwanza; na ukifumbua mdomo wake utaona shekeli ichukue hiyo ukawape kwa ajili yangu na kwa ajili yako.”**

Yesu alitenda muujiza pesa kulingana na uhitaji uliojitokeza kwa ghafla.Pesa ni ya kodi Yesu anaweza kukulipia kodi kimuujiza ikiwa umepungukiwa.

**Luk 5.4—7 “... mkashushe nyavu zenu mvue samaki.Simoni akajibu akamwambia, Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu.**

**Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno,…”**

Yesu alitenda muujiza samaki kwa petro ili ampate Petro afikie maamuzi ya kutubu na kumwamini mungu.Yesu ni mtenda miujiza wokovu wako baada ya kuokoka ukipewa maisha ya miujiza ya Yesu mshukuru Mungu

7. MPONYAJI

Uponyaji ni nini? Ni kuponyeshwa magonjwa sugu yanayotoka na dhambi baada kusamehewa na Mungu/Yesu dhambi zilizosababisha hayo magonjwa **ZAB 103:3** kwa nguvu ya uponyaji ya Mungu au Yesu bila kupewa dawa kwa kuwekewa mikono na Yesu au watumishi wake aliowatuma, au kupakwa mafuta ya uponyaji nao au kwa kutamkiwa neno la uponyaji nao au Yesu/mungu/Roho mtakatifu. Tofauti ya tabibu/daktari na Yesu ni kuwa tabibu hutibu kwa kutoa tiba yaani dawa/mizizi/mimea ya tiba bali Yesu anaponya kwa kuwekea mkono au kutamka Neno la uponyaji.

**Math 4.23 "Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu."**

Yesu ni mponyaji wa magonjwa ya kila namna ktk watu yaliyo sugu na yasiyo sugu mfano Homa na safura,kupooza kiungo kimoja au zaidi, mwili mzima ,ukoma n,k. **"Math 4:24 na wenye kupooza; akawaponya." & "Math 12.13 Kisha akamwambia yule mtu, Nyosha mkono wako; akaunyosha, ukapona, ukawa mzima kama wa pili."**

**"Math 15.30 — 31 Wakamwendea makutano mengi wakimletea viwete, vipofu, mabubu, vilema, na wengine wengi, wakawaweka miguuni pake; akawaponya; hata ule mkutano wakastaajabu, walipowaona mabubu wanasema, vilema wanakuwa wazima, viwete wanakwenda, na vipofu wanaona; wakamtukuza Mungu wa Israeli."**

Yesu ni mponyaji wa ajabu ktk maandiko hapo juu yanatamkwa magonjwa sugu ambayo Yesu aliponya kama ububu,upofu,uwete na ulemavu. Mfahamu Yesu ni mponyaji wa yaliyoshindikana kwa wanadamu na hospitalini. Jifunze je ugonjwa wako una habari ktk biblia mtafute nawe utauona utukufu wa mungu ktk huo kwa asili ya magonjwa ni dhambi kuokoka ni lazima.

## 8. MWALIMU(RABI)

# Yesu ni mwalimu aliyewafundisha waisraeli njia Mungu na ufalme wa mbinguni.

**Yoh 1.38 "Yesu aligeuka, akawaona wakimfuata, akawaambia, Mnatafuta nini? Wakamwambia, Rabi, (maana yake, Mwalimu), unakaa wapi?"**

Yesu ni Mwalimu wa mambo ya mungu yaani rabi wanafunzi wa yohana mbatizaji walimwita hivyo naye hakuwakataza kwa kuwa ndivyo alivyo. Sawa na ktk maandiko hapo juu pengine kutoka na mafundisho yake Yesu ambayo walisikia akifundisha kuhusu mungu au kuambiwa waisraeli wenzao.

**Yoh 3.2 Huyo alimjia usiku, akamwambia, Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.**

Na andiko hili pia linathibitisha Yesu anaitwa mwalimu na Nikodem ambaye alikuwa mwalimu wa Israeli ktk mambo ya mungu ikiwemo torati.Nikodem alimwita Yesu rabi kwa sababu ya mafundisho yake yaliyoambatana na ishara kama kutoa pepo na miujiza .

**"Math 23.8 Bali ninyi msiitwe Rabi, maana mwalimu wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu."**

Yesu ni mwalimu wa mitume kumi na mbili ktk andiko hilo hapo juu Yesu anawakata mtume wasiitwe waalimu bado ni wanafunzi wake hawajahitimu bado hawajabatizwa kwa Roho mtakatifua hivyo wamwite Yesu ndiye mwalimu wao na wanapaswa kuishi kama ndugu.

Yesu alikuwa na huduma ya ualimu wa mambo ya ufalme likiwemo kanisa kutoka kwa Baba yake. Mbinguni. Je una jambo lolote jema unataka kujinza kuhusu Mungu? Mwombe Yesu akufundishe kweli.

# 9. NABII

Nabii ni nani? Ni mtu anayeoneshwa/sikizishwa jambo linaloweza kutukia/kutendwa baadaye na la kweli na Baba yake Yesu au Mungu. Na kweli hutukia unabii hutoka kwa mungu. Tafsiri ya neno nabii ni mwonaji.

Yesu ni nabii mkuu aliyetabiria mitume mabaya yatakayowapata kwa ya kuhubiri injili yake ; Unyakuo wa kanisa na mwisho wa dunia au Dahari. Aliyetabiria waokokao kutambulika kwa ishara na watumishi wake kwa kazi, waokokao kujibiwa maombi yao na kujenga kanisa, ujio wa msaidizi Roho mtakatifu na ikawa kwa waliokoka.

**Yoh 16.2 "Watawatenga na masinagogi; naam, saa yaja atakapodhania kila mtu awauaye ya kuwa anamtolea Mungu ibada."**

**Math 23.34— 35 "Kwa sababu hiyo, angalieni, mimi natuma kwenu manabii na wenye hekima na waandishi; na wengine wao ninyi mtawaua na kuwasulibisha, na wengine wao mtawapiga katika masinagogi yenu, na kuwafukuza mji kwa mji; hivyo ije juu yenu damu yote ya haki iliyomwagika juu ya nchi, tangu damu ya Habili, yule mwenye haki, hata damu ya Zakaria bin Barakia, mliyemwua kati ya patakatifu na madhabahu."**

**Marko 13.9 Nanyi jihadharini nafsi zenu; maana watawapeleka ninyi mabarazani; na katika masinagogi mtapigwa; nanyi mtachukuliwa mbele ya maliwali na wafalme kwa ajili yangu, kuwa ushuhuda kwao.**

**Matendo ya Mitume 9:1 – 2 Lakini Sauli, akizidi kutisha na kuwaza kuwaua wanafunzi wa Bwana, akamwendea Kuhani Mkuu, akataka ampe barua za kuenda Dameski zilizoandikwa kwa masinagogi, ili akiona watu wa Njia hii, waume kwa wake, awafunge na kuwaleta Yerusalemu.** Mistari ya maandiko hayo inathibitisha Yesu ni nabii alitabiri na yakawa mf: mistari ya matendo utimiaji wa nabii zake.

## 10. AMRI YA KUTOA PEPO NA NGUVU ZA GIZA

Yesu ana amri ya kutoa pepo wa kila aina leo twashuhudia kwa jina  lake nguvu za giza hutolewa kama uchawi, uganga wa kienyeji, utendaji wa falme au mamlaka za giza husimamishwa au kuharibiwa.

**"Math 12.28  Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia."**

Yesu alitoa pepo kwa nguvu za Roho mtakatifu yaani nguvu za mungu  amri yake ya kutoa pepo iliambatana na nguvu za mungu . Siyo maneno matupu yenye amri yasiyo na nguvu za mungu.

**"Math 17.18  Yesu akamkemea pepo, naye akamtoka; yule kijana akapona tangu saa ile."**

Andiko hili linashuhudia Yesu ana amri ya kutoa pepo wanaotesa wanadamu.  Kwa mtu uliyeokoka wa kimataifa Yesu yu ndani yako fahamu una amri ya kutoa pepo si wewe bali Yesu aliye ndani yako Marko 16;14-18

**"Marko 1:25—26  Nakutambua u nani, Mtakatifu wa Mungu. Yesu akamkemea, akisema, Fumba kinywa, umtoke.Yule pepo mchafu akamtia kifafa, akalia kwa sauti kuu, akamtoka."**

**"Marko 1.34  Akaponya wengi waliokuwa na maradhi mbalimbali, akatoa pepo wengi, wala hakuwaacha pepo kunena, kwa sababu walimjua."**

**Marko 3.11  Na pepo wachafu, kila walipomwona, walianguka mbele yake, wakalia wakisema, Wewe ndiwe Mwana wa Mungu.**

Kwa mistari michache ya maandiko matakatifu inashudia Yesu alikuwa amri ya kutoa Pepo. Akiwa ndani yako ujue una amri ya kutoa pepo. Kutoa pepo ni sehemu ya maisha ya Yesu alipokuwa ktk dunia. Ukitoa pepo kwa jina lake kama kifafa ufahamu yu ndani yako na yu upande hiyo kazi ya mungu unayofanya.

# 11.HANA DHAMBI

Yesu hana dhambi maisha yake yalikuwa makamilifu mbele za mungu kwa kuitii sauti yake , haikuonekana hila ktk midomo yake wala moyoni.. Pia hakuna mwanadamu aliyeweza kushuhudia kuwa ana dhambi. Wokovu wa Yesu hakuwa dhambi alikuwa mkamilifu ktk kushika yaliyoandikwa ktk torati na yaliyoamriwa na mungu kwa kutumia manabii wake,Kwa kuwa alikuwa hana dhambi chochote chenye asili ya dhambi kama umaskini. Ugonjwa, mapepo. Nguvu za giza uchawi na kazi yoyote ya yule mwovu alikuwa na mamlaka juu ya hizo kama kuziharibu,kuzitoa au kuzibomoa kwa nguvu roho mtakaifu na kwa jina la Baba yake.

**Yoh 8.34—36 "Yesu akawajibu, Amin, amin, nawaambia, Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi.Wala mtumwa hakai nyumbani sikuzote; mwana hukaa sikuzote. Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli."**

Kwa maneno ya kinywa chake ktk maandiko hapo juu Yesu hakuwa mtumwa wa dhambi. Alikuwa huru mbali na dhambi,alikuwa haitumikii dhambi.

**Yoh 8.46 "Ni nani miongoni mwenu anishuhudiaye ya kuwa nina dhambi? Nami nikisema kweli, mbona ninyi hamnisadiki?"**

Kwa maneno ya kinywa chake ktk maandiko hapo juu Yesu hakuwa na dhambi kabisa.

**1 Petro 2:22 – 23 "Yeye hakutenda dhambi, wala hila haikuonekana kinywani mwake.**

**Yeye alipotukanwa, hakurudisha matukano; alipoteswa, hakuogofya; bali alijikabidhi kwake yeye ahukumuye kwa haki."**

Kwa maneno ya kinywa chake ktk maandiko hapo juu Yesu hakutenda dhambi ktk maisha yake hata kama alionewa hakutoa maneno ya hila hila kinywani mwake. Kama umeokoka mtafute Yesu akuweke huru siku zote ktk wokovu wako ndipo utakuwa mwana kweli.

# 12. YESU ANASEMA

Yesu anasema na kondoo wake nao humsikia. Kondoo wake ni watu waliokoka kama wewe mtu wa kimataifa uliyeokoka unaposikia sauti yake itii kama ya mfalme,Bwana au mchungaji wako ujue anakuongoza kukupeleka ktk malisho na mahali yalipo maji yaliyo hai . Kuitii sauti yake ni ya lazima upate kuzipokea baraka zake alizokubariki rohoni bali usipotii ufahamu laana inakufuatilia usiseme wokovu mgumu.

**"Yoh 10.27 Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata.**

**"Yoh 10.28 Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu."**

**"Yoh 10.29 Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote; wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu."**

Wewe ni kondoo wa Yesu mtu wa kimataifa uliyeokoka na Yesu ni Mchungaji wako mwema na Mkuu. Umejaliwa kusikia sauti ya Yesu .Yesu amekuja kuishi nawe ili akujaze uzima tele na kukulinda dhidi ya yule mwovu u mikononi mwa Baba yake ndiye mungu ili baada ya maisha ufike kwake ktk makao aliyoiandaa na kuishi nawe.Umekusudiwa uzima/mema na Mungu na Yesu.Mwombe Yesu siku zote akuongeze kwa sauti yake. Kwa kutii mafundisho yaliyo ktk injili ya mathayo,marko,luka na yohane ya ktk biblia unaitii sauti ya Yesu.

Kama umeokoka na umejaliwa kusikia ya mungu ya rohoni Ukiwa huna dhambi sauti ya Yesu ikisema ktk moyo wako kwa utukufu wa kumuona au kutokumuona hushuhudiwa na roho mtakatifu kuwa anayesema nawe ni Yesu ina Msusumo/msukumo(upendo) yenye pumzi ya uzima au maisha ya milele ya upole na nyenyekevu lazima kuitii usitoe udhuru kwa kutazama yanayokuzunguka au changamoto. Yesu anasema ili awe mchungaji wako yapasa umtii.

# 13. AMEJAA AMANI,FURAHA,UPENDO,HAKI

Yesu amejaa amani ya ufufuo,Furaha ya mbinguni,Upendo wa Baba yake na Haki kinyume cha dhambi.Mfahamu Yesu ewe mtu wa kimataifa uliyeokoka Yesu akiwa ndani yako amani ,furaha,upendo na haki itajidhihirisha ktk maisha yako usistaajabie mshukuru Yesu kwa kuja kufanya makao ndani yako.

- **Amani**

**"Yoh 14.27 Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga."**

**"Yoh 20.21 Basi Yesu akawaambia tena, Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi."**

Yesu amejaa amani akiwa ktk maisha yako unakuwa mwenye Amani sikuzote ni ishara umepatanishwa na mungu dhambi zako zimeondolewa na unafanya ya Yesu na Baba yake yanayompendeza.Amani ya ufufuo wa Yesu hujidhirisha siku ile ulipookoka au unapookoka unapaswa kuitunza kwa kuifuata. Ukiona unatenda jambo ghafla amani ya yesu iliyo ndani yako ikatoweka hata kama ni jema usiendelee kulitenda.

- **Furaha**

Yesu amejaa furaha ya mbinguni.Yesu humfurahisha aliyeokoka kama wewe mtu wa kimataifa kwa kukutendea mema mfano kukuponya,kukutendea miujiza,kukubariki,kukutoa pepo na kukuweka mbali na nguvu za giza, kukuketisha mkono wa kuume wake(roho yako mbinguni na kuitoa ulimwenguni)

- **Upendo:** Yesu akiwa ndani yako kazi alizozifanya utazifanya pia
- **Haki:** Yesu akikuveka vazi lake la haki hutendi dhambi.

## 14. AMEJAA UZIMA TELE

Yesu amejaa uzima tele.Amejaa maisha ya milele ya mbinguni kwa Baba yake humpa aliyeokoka kama wewe mtu wa kimataifa uliyeokoka.

**“Matendo 3:15-16  mkamwua yule Mkuu wa uzima, ambaye Mungu amemfufua katika wafu; na sisi tu mashahidi wake. Na kwa imani katika jina lake, jina lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemwona na kumjua; na imani ile iliyo kwake yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote”**

Ktk maandiko hayo hapo juu Mitume wanamwita Yesu mkuu wa uzima kwa sababu jina lake limesababisha mtu aliye na udhaifu wa kutembea atembee.Pia wao walishuhudia Yesu alivyofufuka na miujiza kadhaa aliyotenda Yesu kabla ya kufa ya Kufufa mtu wana kila sababu ya kumuita mkuu wa uzima kifo kimeshindwa kwa Yesu mbali viwete kutembea ilikuwa miujiza ya kawaida ktk maisha ya Yesu.

**Yoh 5.26  Maana kama vile Baba alivyo na uzima nafsini mwake, vivyo hivyo alimpa na Mwana kuwa na uzima nafsini mwake.**

Yesu amejaa uzima tele aliopewa na Baba yake  ambaye ni Mungu muumbaji.Yeye amepewa na Mungu uzima naye huwagawia wale awatakao hasa waliokoka kama watu wa kimataifa waliookoka.

**Yoh 10.10  Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele**

Kusudi la Yesu kuja ktk maisha yako mtu uliyeokoka wa kimataifa ni kukujaza uzima tele. Huo uzima Yesu hukupa ni wa mwili na Roho. Mbona hujamwomba na Yu ndani yako? Mwombe huo uzima ili akujaze ktk utele usiwe mwenye kupungukiwa.     **Yoh 11.25  Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi;** Uzima akupao Yesu utakufanya uendelee kuishi hata baada ya kufa. Mfahamu Yesu amejaa uzima tele

# 15. MFALME

Yesu ni mfalme lakini ufalme wake si wa dunia hii ijapokuwa Baba yake kaiumba na vyote vilivyomo ndani yake. Yesu alihubiri juu ya ufalme wa mungu ambao ni wa Baba yake ambaye ni Mfalme. Baba yake Yesu amemfanya Yesu mfalme kwa waliokoka na watakatifu waliopo makao amempa sehemu ya ufalme wake amiliki na kutawala.

**"Yoh 12.13 wakatwaa matawi ya mitende, wakatoka nje kwenda kumlaki, wakapiga makelele, Hosana! Ndiye mbarikiwa ajaye kwa jina la Bwana, Mfalme wa Israeli!Naye Yesu alikuwa amepata mwana-punda, akampanda, kama vile iliyoandikwa,Usiogope, binti Sayuni; tazama, Mfalme wako anakuja, amepanda mwana-punda."**

Yesu ni mfalme alitabiriwa na manabii kama Zekaria na Isaya 9:6.

Wewe uliyeokoka mtu wa kimataifa Yesu ni mfalme wako jifunze jinsi ya kumtumia. Sikuzote ktk utawala wa kifalme utii ndio unaohitajika peke yake. Ukifahamu neno lake jifunze kutii ili kumpendeza na kufurahisha mfalme wako Yesu. Akifurahi atakubariki hutakosa baraka yake.

**1Timotheo 6.14—15 kwamba uilinde amri hii pasipo mawaa, pasipo lawama, hata kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo;ambako yeye kwa majira yake atakudhihirisha, yeye aliyehimidiwa, Mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana;**

Yesu ni mfalme wa wafalme chini ya ufalme wa Mungu kuna wafalme ktk maeneo mbalimbali ya ufalme wa mungu. Yesu anawatawala hao wafalme na wewe uliyeokoka ni uzao wa kifalme wa Yesu na sehemu ya huo ufalme wewe ni mwenyeji wa ufalme wa mbinguni/mungu. Uwenyeji uliupata siku ulipookoka. Ufahamu Yesu ni Mfalme kwako mpe moyo wako au maisha yako akutawale na kukutumia kwa kusudi lake..ewe mtu wa kimataifa uliyeokoka.

## 16. MFALME

**Math 2.2 Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia.**

Ktk maandiko matakatifu hapo juu yanashuhudia Yesu ni mfalme aliyetambuliwa na mamajusi nyota yake pindi alipozaliwa na bikira mariamu.

**"Ufunuo Yoh 17.14 Hawa watafanya vita na Mwana-Kondoo, na Mwana Kondoo atawashinda, kwa maana Yeye ni Bwana wa Mabwana, na Mfalme wa Wafalme, na hao walio pamoja naye ndio walioitwa, na wateule, na waaminifu."**

**"Ufunuo Yoh 19.16 Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME, NA Bwana WA MABwana."**

Yesu ni mfalme wa wafalme akiwa ndani yako wewe ni mshindi dhidi ya dhambi na madhara yake yaani laana kama magonjwa, umaskini,kutokufanikiwa, mapepo, uchawi, uganga wa kienyeji na kazi zote za yule mwovu.

⇒ Mfahamu Yesu alivyo akiwa ndani yako madiliko ya kiroho na kimwili yanayotokea ktk maisha yako usishangae kama zile ishara zilioandikwa ktk Marko 16:14-18 kutokea ndani yako,hali ya kushinda dhambi uliyofikiri usingeza acha; maisha ya haki. Kuwa tayari kutumiwa na Yesu ktk kutoa pepo, kuponya hata kutenda miujiza, Baraka ktk shughuli zako,Kusikia sauti ndani yako ya Roho mtakatifu au Yesu kutoka juu mbinguni hadi ktk moyo wako au kukutokea na kuongea nawe au malaika zilizobeba jumbe za ufalme wa mungu/Yesu zikinena ya mbinguni wala si ya ulimwengu. Mshukuru Yesu kwa madiliko jifunze kukaa ktk maombi mwambie Yesu kila siku atumie mwili wako kwa kusudi lake sawa na nguvu za roho mtakatifu zilizo ndani yako..

## 17. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 18. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa Yesu alivyo uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**

Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :

**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 9332

**MWENGE— DAR-ES-SALAAM TANZANIA**



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003  kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034